# Jinsi ya kufikia huduma ya afya nchini Uskoti

Aprili 2011

Access to health care - Swahili

Kijitabu hiki kinatoa maelezo kuhusu jinsi ya kufikia huduma ya afya katika Uskoti. Kinatoa majibu kuhusu maswali ya kupata huduma ya afya unapopitia hali ya utafutaji kimbilio na baadaye.

**Ninaweza kupata usaidizi wa afya katika Uskoti?**

- Ndio, katika Uskoti, huduma nyingi za afya hutolewa na Huduma ya Kitaifa ya Afya (NHS).
- Iwapo wewe ni mtafuta kimbilio au mkimbizi, mengi ya huduma hizi zitaptikana kwako bure.

**Ninawezaje:**

**Kupata huduma ya afya katika Makao ya Kwanza (kwa kawaida utakaa huku kwa wiki 2-4)?**

- Iwapo una hali ya dharura ya kimatibabu, piga simu kwa ofisi ya Huduma ya Kuingizwa Uskoti (SIS) wakati wa masaa ya kazi saa tatu na nusu asubuhi Jumatatu hadi Ijumaa.
- Unapoishi katika Makao ya Kwanza utasajiliwa kwa muda na mmoja wa madaktari katika Kituo cha Matibabu cha Fernbank. Hiki kinapatikana katika 194 Fernbank Street, Springburn, Glasgow, G22 6BD.
- Unapswa kupanga miadi yako na daktari kupitia ofisi ya Huduma ya Kuingizwa Uskoti (SIS)wakati wa masaa ya kazi saa tatu na nusu asubuhi Jumatatu hadi Ijumaa.

**Kufikia huduma ya afya baada ya kupelekwa kwa makao ya muda mrefu (unaojulikana kama utawanyishaji)?**

- Utapewa daktari wa mtaa
- Unapaswa kutumiwa Kadi ya Usajili wa Daktari katika masaa 48 ya kuwasili katika anwani yako. Iwapo hutapokea kadi hii, wasiliana na mkimu wako wa makao.
- Kadi yako ya Usajili wa Daktari hukupa jina, anwani na nambari ya simu ya daktari wako mpya.
- Ni muhimu sana kuwa uende kwa ofisi ya daktari uliyepewa (upasuaji) punde unapopokea Kadi yako ya Usajili wa Daktari ili kukamilisha usajili wako. Utaweza kupata huduma za afya baada ya kukamilisha usajili wako.

Scottish Refugee Council, 5 Cadogan Square, (170 Blythswood Court), Glasgow G2 7PH Tel: 0141 248 9799, Fax: 0141 243 2499,
www.scottishrefugeecouncil.org.uk
Scottish Refugee Council is a charity registered in Scotland.
Registered Charity: SC008639

**Ninawezaje:**

**Kufikia huduma ya afya iwapo nimepewa hali ya ukimbizi au haki ya kubakia?**

- Iwapo utafanikiwa kupata hali ya ukimbizi au haki ya kubakia, unaweza kupata utinzaji wa bure wa afya katika Uskoti na katika Uingereza. Utakuwa umejisajili na daktari wako ila iwapo unataka kubadilisha eneo lako la makazi. Iwapo utahama katika eneo lingine, utaweza kujisajili na daktari wa mtaa katika ofisi yake (upasuaji).

**Kufikia huduma ya afya kama sijapewa hali ya ukimbizi au haki ya kubakia?**

- Iwapo unakata rufaaa dhidi ya uamuzi mbaya wa dai lako la ukimbizi, unaweza kuendelea kupata utunzaji wa bure wa afya mpaka uamuzi utolewe.

- Iwapo dai lako la utafutaji kimbilio umekataliwa, na rufaa zozote dhidi ya uamuzi huo zimeakataa lakini bado uko Uingereza, bado unaweza kupata huduma ya afya kutoka kwa NHS ukiwa bado uko Uskoti.

**Kupata huduma ya dharura ya afya?**

- Iwapo wewe au mtu wa familia yako ni mgonjwa sana au ameumia, unapaswa kwenda katika kitengo cha Ajali na Dharura (A&E) katika hospitali yako ya mtaa. Iwapo ungependa kupelekwa na ambulansi kwa kitengo cha Ajali na Dharura, piga simu kwa **999.** 999 ndiyo nambari rasmi ya dharura ambayo itakuruhusu kuwasiliana na huduma za dharura kwa usaidizi wa haraka; si ya kutumia wakati wa dharura tu.
- Kitengo cha Ajali na Dharura (A&E) katika hospitali hufunguliwa masaa 24 siku 7 kwa wiki
- Hakuna miadi inayotakikana li kuhudhuria kitengo cha Ajali na Dharura katika hospitali lakini kunaweza kuwa na kungoja sana ili kuona daktari au muuguzi.

**Ninapaswa kufanya nini iwapo sijajisajili na daktari?**

Iwapo hujajisajili na daktari, unapaswa kuwasiliana na mkimu wako wa makao au shirika lolote la mtaa la wakimbizi ili waweze kukupa ushauri na jinsi ya kujisajili katika mtaa wako

**Je, ninapaswa kufanya nini kama sijafurahishwa na huduma inayotolewa na NHS?**

Ni muhimu kukumbuka ya kwamba:

- Una haki ya kushughulikiwa kwa heshima, kwa uadilifu na kwa msingi wa usawa na mtu mwingine yeyote wakati wa kufikia huduma ya afya ya NHS.
- Una haki ya kupata mkalimani kwa miadi zako za NHS. Kama unapendelea mkalimani mwanaume au mwanamke, unaweza kuomba hii. Kama hujafurahishwa na mtu uliyepewa akalimani katika miadi yako, unapaswa kumwambia mmoja wa wafanyikazi wa NHS mara moja. Kwa mfano, kama unamjua mkalimani vizuri na huna amani kufichua maelezo ya kibinafsi kwake au kama mkalimani huyo hazungumzi lugha yako mahsusi vizuri ili uweze kuelewa vizuri na kueleweka, unapaswa kumwambia mmoja wa wafanyikazi wa NHS.
- Una haki ya kuomba daktari uliyepewa abadilishwe (GP) na upewe daktari mwingine katika ofisi hiyo (chumba cha daktari). Kwa mfano, kama wewe ni mwanamke na ungependa kumwona daktari au mtaalamu mwanamke, unaweza kuomba hii. Ombi lako linapaswa kushughulikiwa kama inawezekana.

Kama hujafurahishwa na huduma inayotolewa na NHS au unaamini kwamba umepokea huduma duni au isiyotosha kutoka kwa yeyote anayefanya kazi katika NHS, una haki ya kutoa malalamiko. Kutoa malalamiko **hakuaathiri** hadhi yako ya uhamiaji au madai yako ya hifadhi.

Kwa maelezo zaidi kuhusu kutoa malalamiko, unapaswa kuwasiliana na huduma ya ushauri ya eneo lako au idara za malalamiko za NHS, nambari ya simu 0141 201 4500 au barua pepe complaints@ggc.scot.nhs.uk. Kuna pia mabango ya bluu angavu ya 'Maoni, Hoja na Malalamiko' yaliyoonyeshwa katika majengo yote ya NHS ambayo yanatoa maelezo zaidi kuhusu kutoa malalamiko.